# LONDA

## BENIN HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE



# RIPORT YA 2020

www.paradigmhq.org

PARADIGM INITIATIVE

@ParadigmHQ

# LONDA

## BENIN HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

**Imechapishwa na Paradigm Initiative**
374 Borno Way, Yaba, Lagos, Nigeria
Email: media@paradigmhq.org
www.paradigmhq.org

Iliyochapishwa mnamo Aprili 2021

Ripoti iliyotolewa na Sinatou Saka
Timu ya Uhariri: 'Gbenga Sesan, Kathleen Ndongmo, Koliwe Majama, Margaret Nyambura Ndung'u, Mawaki Chango, Nnenna Paul-Ugochukwu and Thobekile Matimbe.
Ubunifu na Luce Concepts

This publication may be reproduced for non-commercial use in any form provided due credit is given to the publishers, and the work is presented without any distortion.

Copyright © 2021 Paradigm Initiative

Creative Commons Attribution 4.0 International (CC BY 4.0)



# LONDA

**BENIN HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI**

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

## YALIYOMO

UTANGULIZI 1

MIUNDOMBINU YA MTANDAO 2

MFUMO WA KISHERIA WA MTANDAO 2


UHURU WA KUJIELEZA KWENYE MAJUKWAA YA KIDIJITALI 3

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 4

Asasi za kiraia zinaendelea kufanya kazi ili kuendeleza haki za dijitali na ujumuishi barani Afrika, kuhakikisha njia bora zinapitishwa katika sera na sheria. Ripoti hii inachambua hali ya haki za dijitali na ujumuishi nchini Benin, ikichunguza ukiukaji na mapungufu, ikiangazia utumiaji na utekelezwaji wa sera na sheria, ikiangazia hatua muhimu na kutoa mapendekezo kwa mandhari ya dijitali nchini Benin. Pamoja na ripoti kutoka nchi 20, toleo hili linaangazia kati ya maswala mengine, pengo la kidijitali lililozidishwa na janga la COVID-19 na kufichua ukiukaji kwenye nyanja tofauti kama vile faragha, ufikiaji wa habari, na uhuru wa kujieleza na msingi wa sheria na sera ulioelezewa vizuri .

PARADIGM INITIATIVE

@ParadigmHQ



Nchi ya Benin, imepakana Kaskazini na Niger, Mashariki na Nigeria, Magharibi na Togo na Kusini na Bahari ya Atlantiki, Benin iko katikati mwa Afrika Magharibi. Nchi ina mikoa 12, na eneo la ardhi ni la ukubwa wa 114, 764 km2.

UTANGULIZI

# HAKI ZA DIJITALI NA UJUMUISHAI YA NCHI YA BENIN

Mnamo mwaka 1995, Nchi ya Benin ilijiunga na ulimwengu wa mtandao wakati wa mkutano wa sita wa Wakuu wa Nchi na Serikali.[1]

Hivi leo, wavuti wa rununu wa 3G umefikia wastani wa asilimia 60 ya idadi ya watu, (Mpango Mkuu wa TEHAMA na mawasiliano ya simu huko Benin, Juni 2017). Kulingana na takwimu zilizochapishwa na ARCEP, kiwango cha kupenya kwa mtandao ni asilimia 48,02.

**60%**
**ya idadi ya watu imefunikwa na mtandao wa rununu wa 3G**

Kulingana na takwimu ya Muungano wa Watengenezaji Programu za Kompyuta nchini Benin (Association of Developers and Coders in Benin), kuna watengenezaji kati ya 500 hadi 600, Mnamo mwaka 2017, Faharisi ya Maendeleo ya Mtandao ya Benin, yaani Benin's Internet Development Index (IDI) ilikuwa 1.94, na kuifanya nchi kufikia namba 161 ulimwenguni , ikiwa nyuma ya Togo, Mali, Senegal na Ivory Coast. Katika nchi ya Benin kiwango cha muunganisho wa rununu kwa mwaka 2017 kilikuwa 37.3. Kama ilivyo kwa Faharisi ya Utayari wa Mtandao, Benin ni ya 128 ulimwenguni kati ya nchi 139 zilizo na faharisi ya 2.9 mnamo 2016.

1. https://www.google.com/url?q=https://cursus.ebsi.umontreal.ca/vol6no1/bai.html%23:~:text%3DL%27histoire%2520d%27Internet%2520a,couvrir%2520les%2520activit%25C3%25A9s%2520du%2520Sommet&sa=D&source=editors&ust=1617863321683000&usg=AOvVaw0O3uL3QW8t4dfEZHmeaPv9

## MIUNDOMBINU YA MTANDAO

Baada ya kupitishwa kwake mnamo 2016, Andiko la Sera la Sekta (SPS)[2] limekuwa ni mwongozo wa kidijitali nchini Benin. Kulingana na mamlaka ya taifa, kuhusu kasi kubwa ya mtandao, mtandao wenye Zaidi ya kilomita 2000 zilizounganishwa na mkonga wa taifa umeunganishwa kwenye maeneo 60 na manispaa 77.

Kutokana na vyanzo vya uhakika vya taarifa, mwendeshaji mkuu wa sasa, Benin Telecom Infrastructures (BTO) amepunguza gharama hadi asilimia 50 kwa wastani wa uwezo wa hadi 40 kwenye miji mikuu ya wilaya na zina uwezo wa kasi ya 50 Mbps ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa huduma tatu zikiwemo: Vituo vya Jamii vya Kidijitali, vituo vya bure vya Wi-Fi kwenye baadhi ya maeneo ya umma yenye uwezo wa kasi ya 4 Mbps na watumiaji wa huduma kwa watu binafsi ikiwa na uwezo wa kasi ya 36 Mbps.

## MFUMO WA KISHERIA WA MTANDAO

Sheria namba 2017-20 mnamo Aprili 20 2018 ya Kanuni za kidijitali nchini Benin ni sheria pekee inayozungumzia sekta ya kidijitali Benin tangu 2018. Kanuni ya Kidijitali inahusika na mawasiliano ya kielektroniki, mtandao na huduma. Ina mwongozo unaotumika kwa waendeshaji wa mitandao na shughuli za mawasiliano ya kielektroniki. Zana za kielektroniki na Hati (Documents), Muswada unaelekeza uaminifu kwa watoa huduma na kuongozwa na sheria hii, ambayo pia inatoa maelekezo ya kulinda taarifa za kibinafsi na zile zinazohusiana na Makosa ya Mtandao na Ulindaji wa Mtandao.

Ukilinganisha na Sheria namba 2014 ya mnamo Julai 9 2014, upeo wa sheria mpya ya Kanuni za Kidijitali ni mpana. Haibebi tu sasisho jipya kuhusiana na shughuli zinazo husisha mtandao wa mawasiliano ya kielektroniki, huduma na ulindaji data za kibinafsi, bali inatoa mwongozo wa kisheria unao tumika kwenye biashara na mawasiliano ya kimtandao, makosa ya mtandao na vikoa kwa kipindi cha nyuma hazikuwa na sheria. Ina ratibu sheria ya makosa ya kimtandao ya jinai na makosa yaliyofanyika mtandaoni.

Katika ripoti ya Mwisho, ARCEP (Mamlaka ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta) ina eleza kwamba mtandao usioegemei upande wowote ni kanuni kuu ya Jamhuri ya Benin. “Waendeshaji mtandao wanaotoa huduma za mtandao hawafanyi hatua za kudhibiti mtiririko” Kiuhalisia wanatakiwa kuacha kuuzima, kuupunguza kasi, kuufanyia marekebisho, kuuzuia, kuushusha hadhi au kubagua dhidi ya maudhui, maudhui maalumu na huduma zitolewazo.

Ulindaji wa falagha ni moja ya masilahi mapana kwa wabunge wa Benin. Mamlaka ya ulindaji wa Data za Kibinafsi (APDP) ipo ili kuchukua hatua za kisheria zinazohusiana na matakwa ya kisheria yaliyo na ulindaji wa data binafsi. Tangu kuundwa kwake mnamo 2009, imesha thibitisha maamuzi 300 ya ukusanyaji na ufutaji wa data binafsi na kusajili takribani malalamiko.



2. Sector Policy statement – Strategic orientations 2021 in the digital economy sector: https ://numérique. gouv.bj/images/DPS.pdf

## UHURU WA KUJIELEZA KWENYE MAJUKWAA YA KIDIJITALI.

Kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi, mtandao ulikatwa siku nzima wakati wa uchaguzi wa bunge, mnamo April, 28 2019. “Maamuzi ya kuzima mtandao na mitandao ya kijamii kwa siku nzima wakati wa uchaguzi ni uvunjaji wa haki ya kujieleza” anathibitisha Francois Patuel, Mtafiti kutoka Amnesty International Afrika ya Magharibi.

Mwandishi wa Habari wa zamani, Aziz Imorou alikamatwa mnamo Septemba 17 2020[3] baada ya kuchapisha nakala kwenye Facebook ambayo ilikashifu kitendo cha madai ya unyanyasaji dhidi yake na mlinzi wa Armand Ganse, Mkurugenzi Mkuu wa Société de Gestion des Marches Autonomes (SOGEMA), kampuni inayomilikiwa na serikali inayosimamia masoko ya umma. Aliiambia West Africa Media Foundation kwamba alishambuliwa na mlinzi wa Bwana Ganse wakati akipiga picha za gari lililogonga mwendesha baiskeli wa kibiashara. Wakati alikuwa akipiga picha hizo, watu wanne walimshambulia na kumpokonya simu yake.

Siku moja baada ya kuchapishwa kwenye Facebook, Aziz Imorou aliitwa Ofisi Kuu ya Ukandamizaji wa Uhalifu wa Mtandaoni (OCRC) kufuatia malalamiko yaliyowasilishwa na Mkurugenzi wa SOGEMA. Baada ya kumhoji, Aziz Imorou alifikishwa mbele ya mahakama ya kesi ya mwanzo huko Cotonou. Bila hata ya kutoa uamuzi, jaji alimrudisha mshtakiwa katika Gereza la Kiraia la Cotonou kwa kashfa. Mahakama ilimwachilia huru bila mashtaka kwa misingi ya shaka la manufaa mnamo Oktoba 6 2020.

Hii sio kesi ya kwanza nchini. Mwendesha mashtaka wa Benin, Mario Metonou, alianzisha kukamatwa, kushtakiwa na kufungwa kwa Ignace Sossou, mwandishi wa habari wa Benin Web TV mnamo Desemba 2019.[4] Mwendesha mashtaka alilalamika kwamba ile tweet, kutoka kwa mwandishi wa habari huyo anayedai kunukuu maneno yaliyonenwa kwenye mkutano, haikuwa sahihi. Alifungwa mnamo Disemba 24 2019, Ignace Sossou akatolewa mnamo Juni 24 2020 baada ya kukata rufaa kwa mafanikio dhidi ya kifungo chake cha miezi 18 gerezani.

Mnamo Julai 8 2020, Mamlaka Kuu ya Usikilizaji na Mawasiliano ya Benin ilitoa taarifa, ikitishia tovuti “kusitisha machapisho yote”. Mwisho kusingekuwa na idhini ya uchapishaji iliyotolewa na chombo cha udhibiti.

Uamuzi huu unakuja wakati maafisa kadhaa wa vyombo vya habari, wakiwa wameomba idhini yao ya kuchapishwa kwa miezi kadhaa, hawajawahi

> ***“Mamlaka ya ulindaji wa Data za Kibinafsi (APDP) ipo ili kuchukua hatua za kisheria zinazohusiana na matakwa ya kisheria yaliyo na ulindaji wa data binafsi.”***

3. https://www.google.com/url?q=https://www.24haubenin.info/?Le-journaliste-Aziz-Imorou-arrete&sa=D&source=editors&ust=1617864857954000&usg=AOvVaw0nne_l1HsaFWp_2MPLyZtl
4. https://www.google.com/url?q=https://www.liberation.fr/planete/2020/01/23/journaliste-beninois-emprisonne-ce-qu-il-s-est-passe-est-une-aberration_1774894/&sa=D&source=editors&ust=1617863321688000&usg=AOvVaw1wuzTJaLlBwzblGVHcVXKN

kupokea jibu kutoka kwa HAAC. Hatua hii haswa ingezuia kuenea kwa habari potofu kwenye mtandao.

Kutokana na Jeune Afrique, msemaji wa Mamlaka Kuu ya Benin ya Usikilizaji na Mawasiliano (HAAC),[5] huibua kupatikana kwa idhini ya awali ya kudai hadhi ya msaada wa vyombo vya habari, haswa kupitia "maswali ya maadili" maadili ambayo haijulikani kabisa na haswa ikiwa tafiti hizi zinafanywa na watu huru.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Mwaka wa 2020 ulikuwa ni wa kukamatwa kwa waandishi wa habari wawili kwa shughuli zao za mtandaoni. Uamuzi wa hivi karibuni wa Mamlaka Kuu ya Usikilizaji na Mawasiliano, inaonesha kurudi nyuma kwa uhuru wa kimsingi mtandaoni.

Kwa mtazamo wa kiufundi, jukwaa la malipo la kawaida lililozinduliwa hivi karibuni, mwingiliano kati ya huduma ya pesa za rununu na benki, jukwaa la ushirikiano wa mifumo ya habari ya serikali na uzinduzi wa huduma zaidi ya 250 za huduma- mtandao, ni mifano mingi ambayo inashuhudia maendeleo ya kutawaliwa kikamilifu na serikali katika maisha ya kila siku nchini Benin. Haki za dijitali, zilizounganishwa na uhuru wa kujieleza, kwa ubora na uimara wa kiufundi wa miundombinu, kwa suala la usalama, inapaswa kuwa kiini cha mabadiliko ya kidijitali ya Benin, kama mtaalam Pierre Dandjinou anatukumbusha.

Pia, ripoti ya shughuli ya mnamo 2016 ya CNIL Bénin wa zamani (APDP ya sasa) inaonyesha kwamba: "kwa visa vingi, ukiukwaji wa sheria unaonekana hapa na pale katika rufaa chafu zinazohusu ukusanyaji na ujanja wa wafanyakazi wa data ya kibinafsi, hupata chanzo chao kupitia ujumbe wa kijinga ambao unaunda taharuki ya jambo na hiyo ni hatari ".

Kwa hivyo itakuwa busara, kama mwanasheria Christine Tossavi anapendekeza, kuongeza ulindaji wa data ya kibinafsi katika kampuni kwa kusasisha nambari ya kazi ili kuzingatia utumiaji wa zana za TEHAMA na kusasisha maarifa ya wakaguzi wa kazi na mahakimu juu ya matumizi ya Nambari ya kidijitali ya Benin. Ushirikiano kati ya APDP na Kurugenzi ya Kazi itakuwa ina manufaa makubwa katika kuhifadhi haki ya mfanyakazi ya faragha katika kizazi cha kidijitali.

Mfumo wa kisheria uliopo haupaswi kuwa wa kisiasa zaidi kwa kusababisha hasara kwa raia na watumiaji wa mtandao. Raia wote lazima wawe sawa mbele ya sheria, hakuna mtu anayeweza kutumia kifungu cha kisheria kwa maslahi yake mwenyewe.

5. https://www.google.com/url?q=https://www.jeuneafrique.com/1015920/societe/chronique-au-benin-les-medias-en-ligne-sous-pression/&sa=D&source=editors&ust=1617864857963000&usg=AOvVaw2hacGsUotYohtNVcy_RZk6

# LONDA

**BENIN HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI**

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

PARADIGM INITIATIVE

**Paradigm Initiative**

374 Borno Way, Yaba, Lagos, Nigeria

Email: media@paradigmhq.org

www.paradigmhq.org

@ParadigmHQ